# Bandari ya Kilwa fursa muhimu kwa ulinzi wa mazingira baharini

Na MBARAKA KAMBONA, *Kilwa*

SERIKALI ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanaweka mazingira safi na salama kwa wavuvi nchini, ambapo imesaini mkataba wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa.

Bandari hiyo inajengwa na Kampuni ya Ujenzi ya China Habour Engineering (CHEC), ambapo zaidi ya sh. bilioni 266.79 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo itakayokuwa na uwezo wa kuhifadhi tani elfu 60 za mazao ya uvuvi kwa mwaka.

Kwa mujibu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, bandari hiyo ikikamilika na kuanza kazi inatajwa kuwa ndio itakuwa bandari kubwa zaidi kuwahi kujengwa katika ukanda wa Bahari ya Hindi wa pwani ya Afrika Mashariki.

Akizungumza katika makabidhiano iliyofanyika katika eneo la ujenzi lililopo wilayani Kilwa, mkoani Lindi, Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah anasema kwa miaka mingi serikali imekuwa ikipoteza mapato mengi kwa sababu ya ukosefu wa bandari ya uvuvi.

Anasema uwepo wa bandari hiyo utasaidia kuruhusu meli kubwa zinazofanya uvuvi katika bahari kuu kutia nanga, kuwepo kwa bandari hiyo kutawezesha nchi kunufaika na fursa nyingi za uvuvi katika ukanda wa bahari kuu.

"Uwepo wa bandari hii utasaidia kuongeza uwekezaji katika sekta ya uvuvi na kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla pamoja na kulinda uhifadhi wa mazingira kwa kuwa uwepo wa bandari ni chachu ya kufanya uvuvi katika misingi thabiti," anasema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack anawataka wananchi wa Wilaya ya Kilwa kujiepusha na vitendo kuhujumu ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Kilwa, ili mradi huo ukamilike kwa wakati uliopangwa na kunufaisha wananchi na Taifa kwa ujumla.

"Niwaombe wananchi wote tuwe walinzi wa shughuli zote zitakazofanyika katika mradi huu, asitokee mtu sasa akaanza kudokoa vifaa vya ujenzi hapa, tutachelewesha mradi huu kukamilika kwa wakati," anasema Zainab.

Anaongeza kwa kusema kuwa hategemei kuona mkandarasi analalamika kwamba kuna watu wanafanya vitendo vya wizi katika mradi huo, huku akiwaomba wananchi wote kutoa ushirikiano kwa wajenzi hao ili mradi huo ukamilike na manufaa yaanze kupatikana mapema kama ilivyokusudiwa.

Anasema kwa muda mrefu kazi ya uvuvi imekuwa ikiendelea wilayani humo, lakini manufaa makubwa bado hayajapatikana kutokana na uvuvi huo kuwa na vitendea kazi duni, lakini kwa ujenzi wa bandari hiyo utasaidia kuinua shughuli za uvuvi na soko la samaki kutoka Kilwa litafunguka zaidi.



KATIBU Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayesimamia sekta ya Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah (kushoto) akimkabidhi mkataba wa ujenzi Meneja Mkuu, Kampuni ya ujenzi ya China Habour Engineering (CHEC), Cheng Yongjian (kulia).

> "Niwaombe wananchi wote tuwe walinzi wa shughuli zote zitakazofanyika katika mradi huu, asitokee mtu sasa akaanza kudokoa vifaa vya ujenzi hapa, tutachelewesha mradi huu kukamilika kwa wakati,"
>
> **Mkoa wa Lindi, Zainab Telack**

### WAZIRI NDAKI ATOA NENO

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki anasema anautaka uongozi wa Kampuni ya CHEC, ambao ndio wamepewa majukumu ya ujenzi wa bandari hiyo kuhakikisha ujenzi wake unakamilika ndani ya muda uliopangwa kwa sababu fedha kwa ajili ya kufanya kazi hiyo zipo.

"Serikali inataka kuona mradi huu unaanza kufanya kazi kwa haraka, kwa kuwa bandari hii ni muhimu mkubwa kwa maslahi mapana ya nchi. Utakuwa msaada katika uhifadhi mazingira ya bahari na hata kuwa na uwezo mkubwa wa kuzalisha samaki wengi," anasema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Dk. Christina Ishengoma, anasema wizara kuhakikisha wanamsimamia vyema mkandarasi aliyekabidhiwa kujenga bandari hiyo, ili kukamilika kwa wakati.

Naye, Meneja Mkuu wa Kampuni ya Ujenzi ya China Habour Engineering (CHEC), ambayo imepewa zabuni ya ujenzi wa bandari hiyo, Cheng Yongjian alishukuru serikali kwa kuwaamini na kuwapa kazi hiyo na kusema kuwa watatekeleza kwa wakati na kuhakikisha ndani ya miezi 24 watakabidhi mradi huo kwa Serikali ukiwa umekamilika.

Wananchi wa Kilwa Adam Selemani na Rajab Abdallah, ambao wote ni wavuvi walionyesha kuwa na matumaini makubwa na mradi huo huku kwa nyakati tofauti, wakisema watahakikisha wanashirikiana na wajenzi wa mradi huo ili uweze kukamilika kwa wakati.

Selemani anasema ujenzi wa bandari hiyo, utakuwa na faida kubwa kwa wavuvi wa maeneo hayo kwa kuwa sasa shughuli zao zitakuwa zinafanyika rasmi na hata kuondoa ufanyaji wa shughuli za uvuvi katika maeneo yasiyokuwa rasmi.

"Tunampongeza Rais Samia kwa hili, hii ni hatua kubwa kwetu kwa kuwa mradi huu utakuwa wa kisasa na utazingatia mazingira yote muhimu yanayotakiwa katika Bandari za Uvuvi na kusaidia kuboresha shughuli zao kuliko ilivyo hivi sasa," anasema.

Naye, Abdallah anasema uvuvi utafanyika kwa kisasa zaidi na nina uhakika ule uharibifu wa mazingira ya bahari hivi sasa utaondoka, maana ujenzi wa bandari hiyo utasaidia kuleta mafanikio makubwa kwa nchi na kuleta mafanikio makubwa kwa nchi.



KATIBU Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayesimamia sekta ya Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah (kushoto) na Meneja Mkuu, Kampuni ya ujenzi ya CHEC, Cheng Yongjian (kulia) wakisaini nyaraka za makubaliano ya ujenzi wa bandari ya uvuvi ya Kilwa. Katikati ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki kushoto kwa Waziri ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Dk. Christina Ishengoma.

CamScanner

Dk. Stephen Nindi, alisema hayo



Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zaineb Abdallah (kushoto), akimweleza jambo Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, katika hafla fupi ya kuzindua na kukabidhi jengo jipya kwa Kikundi cha Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi cha Dunda (BMU) iliyofanyika wilayani Bagamoyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Bagamoyo district commissioner Zainab Abdallah (L) briefs Livestock and Fisheries minister Mashimba Ndaki at yesterday's handing over in Bagamoyo of a newly completed Beach Management Unit building to Dunda Fisheries Resource Protection Group. Photo: Guardian Correspondent

# Govt to loan 300 boats to fishermen for deep sea fishing

By Guardian Reporter, Bagamoyo

LIVESTOCK and Fisheries Minister Mashimba Ndaki has said the government plans to empower fishermen with modern fishing gear including boats to enable them engage in deep sea fishing to increase catches and enhance their economic wellbeing.

Ndaki made the remarks here on Tuesday at a brief event to launch and hand over a new building to the community based Beach Management Unit (BMU) for Dunda for enhancing security of ocean resources along the Indian Ocean Coast.

Mashimba said the government wants to increase fisheries products and that is why President Samia Suluhu Hassan has increased the Fisheries Budget for FY 2022/23 with some of the money to be used to purchase more than 300 boats to be loaned to fishermen to improve their activities.

He added that the boats will help fishermen to fish in deep sea to harvest big catches to enable fish processing plants to work to their full capacities different from now when many factories perform below installed capacity.

The minister also called on the people to support government efforts in fighting illegal fishing activities stressing that the task is not for the ministry alone, but for everyone.

"Fish is nutrition, fish is money, fish is business and fish is employment, we should work together to fight illegal fishing," he added.

He also called on leaders of BMUs to adopt ethical behaviour and avoid corruption and favouritism as these contribute to illegal fishing.

Meanwhile, Bagamoyo District Commissioner, Zainab Abdallah thanked the government on how it has mobilised itself to empower fishermen, saying through the plan fishermen in her district will greatly benefit.

# Serikali kuwawezesha wavuvi vifaa vya kisasa

**Na Mbaraka Kambona**, PWANI

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema serikali imejipanga kuwawezesha wavuvi vifaa vya kisasa ikiwamo boti kuvua samaki kwenye kina kirefu ili waongeza uzalishaji wa bidhaa hiyo, kuinua uchumi wao na kukuza Pato la Taifa.

Ndaki alibainisha hiyo wakati wa hafla fupi ya kuzindua na kukabidhi jengo jipya kwa Kikundi Shirikishi cha Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi cha Dunda (BMU) kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa rasilimali za bahari katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi iliyofanyika wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani, Julai 5, 2022.

Alisema serikali inataka kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi na ndiyo maana Rais Samia Suluhu Hassan ameongeza bajeti ya Sekta ya Uvuvi ya mwaka 2022/2023 na sehemu yake itatumia kununua boti zaidi ya 300 ili wakopeshwe wavuvi na kuboresha shughuli zao.

Pia boti hizo zitasaidia wavuvi kwenda katika kina kirefu na kuvuna mazao mengi ya samaki na kufanya viwanda vya kuchakata samaki kufanya kazi kwa uwezo wake tofauti na ilivyo sasa viwanda vingi vinafanya kazi chini ya uwezo uliosimikwa.

Waziri Ndaki aliwataka wananchi kuunga mkono juhudi za serikali kupiga vita uvuvi haramu huku akisisitiza kuwa kazi hiyo sio ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi pekee bali ni ya kila mmoja.

"Samaki ni lishe, samaki ni pesa, samaki ni biashara na samaki ni ajira, tushirikiane kupiga vita uvuvi haramu," alisema.

Aliwataka viongozi wa Vikundi Shirikishi vya Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi kuwa waadilifu na kujiepusha na vitendo vya rushwa na upendeleo kwa kuwa ndiyo chanzo cha uvuvi haramu.

Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainabu Abdallah, alishukuru serikali ilivyojipanga kuwawezesha wavuvi akiamini kuwa kwa mipango hiyo wavuvi katika wilaya yake watanufaika kupitia shughuli zao hizo.

**"Samaki ni lishe, samaki ni pesa, samaki ni biashara na samaki ni ajira, tushirikiane kupiga vita uvuvi haramu," alisema.**

# TAV… wa …

**Na Ashton Balaig…**
MOROGORO

TAASISI ya … Wanyamapo… nia (TAWIR… migogoro … adamu na wanyam… kana na shughuli … mu kuvamia katika … asili ya mapito ya w… maarufu kama shor…

Imesema ili mi… iweze kumalizika … serikali kwa kush… sekta binafsi na v… habari, ikaweka … pamoja ikiwamo … jamii umuhimu wa… sha wananchi … umuhimu wa maen…

Mtafiti Mkuu kut… Dk. Stephen Nindi, a…



Mkuu wa Wilaya ya … hafla fupi ya kuzind… ka wilayani Bagamo…

# Mahal…

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya … kupitia Kituo Jum… Masuala ya Familia … Temeke, jijini Dar … ina mpango wa … mashauri saa 24 ili w… waendelee na maju… muda wa kazi.

Hayo yamesemwa … Mkuu wa Kitengo ch… sho ya Mahakama, … Rumisha, wakati Be… nia ilipotembelea ba… hakama katika mao… 46 ya Sabasaba, Dar …

Dk. Rumisha alise… ya kuwapo kwa ki… kimepokea kesi nyi… ya uendeshaji wa … hayo umekuwa na ch…

The Guard

Digital +255 745 700 710 LIKE & FOLLOW US

Tsh 1,000, Kenya sh100 TANZANIA

**National Pg 4**
Govt to empower fishermen with boats

